Kanuni hizi, {East African Organic Product Standard (EAOPS)} zimejadiliwa na wadau wa kilimohai kutoka kanda hii wakishirikiana na serikali za Kenya, Uganda na Tanzania na kuidhinishwa kutumika katika nchi hizi. Kanuni hizi zimebuniwa kulingana na kanuni zingine za kimataifa na zinalenga kurahisisha biashara katika kanda hii kwa kiwango sawa na ilivyo katika mataifa makuu ya ulimwengu. Zaidi na hayo, kanuni hizi zitawezesha biashara ya bidhaa za kilimohai kwenye masoko muhimu ya kimataifa kama vile Jumuia ya Ulaya na Marekani. Kanuni hizi zitawezesha mataifa ya Jumuia ya Afrika Mashariki kuongea kwa sauti moja wanapouza bidhaa zao katika masoko ya kimataifa.

Unawezaji kutambua bidhaa za kilimohai kutoka eneo hili?

Bidhaa zote za kilimohai kutoka kanda ya Afrika Mashariki ambazo zimethibitishwa kwamba zinazingatia kanuni za EAOPS zimetiwa alama ya ubora. Alama hii inamhakikishia mteja kwamba bidhaa hizi ni bora kwani zimekuzwa na kutengenezwa kufuatia kanuni za EAOS. Ili kuhakikisha kwamba kanuni hizi zinafuatiliwa, wakulima na watengenezaji wa bidhaa hizi hukaguliwa na mashirika huru kwa kufuata utaratibu wa hali ya juu ili wapate ithibati ya kilimohai. Kuna mashirika mbali mbali katika kanda hii yanoyotoa ithibati kwa wakulima wa kilimohai. Baadhi ya mashirika haya ni kama vile:

Tancert, BioInspecta, Africert
Encert, Ugocert, Ecocert
IMO Ceres na Soil Association

Kwa maelezo zaidi wasiliana na

KOAN
Mtandao wa Kilimohai Kenya (KOAN)
S.L.P. 72461 00200, Nairobi
Simu: 254 20 8566172 / 3 \4 • Kipepesi: 8566175.
Barua Pepe: Koansecretariat@elci.org

NOGAMU
Asasi ya Uendelezaji Kilimohai Uganda (NOGAMU)
S.L.P. 70071, Kampala
Barua Pepe: admin@nogamu.org.ug

TOAM
Asasi ya Uendelezaji Kilimohai Tanzania (TOAM)
S.L.P. 70089, Dar es salaam
Barua Pepe : kilimohai@bol.co.tz

KILIMOHAI ORGANIC

Naturally Nurtured

Chakula kilichokuzwa kwa misingi asilia

Je, una shaka na chakula unachotumia?

Je, unafadhaishwa na jinsi unavyomtembelea daktari wako mara kwa mara?

Je, una wasiwasi na jinsi inavyokubidi kutumia dawa za tiba mara kwa mara?

Mtu ni Chakula

Unaweza kuishi maisha yenye afya kwa kula chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo hai.

Umuhimu wa kutumia chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimohai

Chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo hai kina manufaa mengi kushinda chakula kingine cha kawaida. Baadhi ya manufaa haya ni:

1. Usalama

Chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo hai ni salama. Hakina sumu kali zinazotokana na unyunyizaji wa dawa na utumizi wa mbolea za kemikali. Masalio ya dawa hizi za kemikali yanapatikana kwenye bidhaa ambazo tayari zimevunwa na yanadhuru afya yako. Kemikali hizi zinaposombana mwilini kwa muda mrefu, zaweza kusababisha magonjwa yenye tabia ya kuchipuza mara kwa mara baada ya kutibiwa. Kemikali hizi huweza kungia kwenye mito, chemichemi za maji na hata kwenye maji yaliyo chini ya ardhi, hivyo kuchafua vyanzo muhimu vya maji. Kilimohai huzingatia kuweko kwa mazingira safi, yaliyolindwa kutokana na madhara ya ukataji holela wa misitu, mmomonyoko wa udongo, na kutoweka kabisa kwa jamii fulani za wanyama na mimea.

Kanuni za kilimo hai hazikubali bidhaa za kilimo kufanyiwa mabadiliko ya kizazi kupitia utafiti mamboleo unaolenga kubadilisha chembe chembe za uzazi.

2. Afya nzuri

Chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo hai humpatia mtu afya nzuri. Chakula hiki kina vitamini nyingi muhimu, madini, na lishe bora ambazo hazipatikani katika vyakula vingine vilivyokuzwa kwa mbinu za kawaida zinazotumia dawa na mbolea za kemikali. Vitamini na madini haya muhimu huimarisha kizazi cha wanyama na binadamu. Kilimohai ni dhibitisho tosha kwa afya ya jamii.

3. Ubora wa bidhaa

Chakula kilichokuzwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo hai kina ladha tamu ya kupendeza. Mboga na matunda yake yana maji mengi, utamu asilia na lishe bora. Chakula hiki huwa kimefanyiwa utafiti wa hali ya juu ili kudhibitisha ubora wake. Wakulima wanapozingatia kanuni za kilimo hai, ubora wa bidhaa unadhihirika.

Je, nini maana ya kilimohai?

Kilimohai ni utaratibu wa kilimo unaolinda afya ya binadamu, wanyama na mazingira kwa kupunguza madhara ya sumu inayotokana na utumizi wa dawa na mbolea za kemikali. Dawa na mbolea hizi huishia kwenye ardhi, hewa, maji na chakula na zimehusishwa na kuenea kwa magonjwa kama vile saratani, pumu na mengineyo. Kilimohai huwezesha mifugo kudumisha tabia zao asilia.

Kanuni za kilimo hai hazikubali bidhaa za kilimo kufanyiwa mabadiliko ya kizazi kupitia utafiti mamboleo unaolenga kubadilisha chembe chembe za uzazi. Aidha, kanuni hizi haziruhusu kuongezwa kwa damu na dawa katika chakula cha mifugo ili kuwawezesha kukua kwa haraka.

Bidhaa za kilimo hai ni zile ambazo zimekuzwa na kutengenezwa kufuatana na utaratibu unaozingatia kanuni za kilimohai na unaojiepusha na utumizi wa dawa na mbolea za kemikali. Ili bidhaa ziweze kuidhinishwa kama za kilimohai, ni lazima ziweze kuzingatia kanuni na masharti fulani wakati zinapokuzwa au kutengenezwa. Mkulima anayezingatia kanuni hizi za kilomohai hupewa cheti cha thibitisho nazo bidhaa zenyewe huwekwa alama fulani kumhakikishia mteja ubora wake.

Thibitisho la ubora katika kilimohai

Kabla ya bidhaa kupitishwa kuwa ni za kilomohai, ni lazima zifikie viwango fulani vya ubora. Bidhaa hizi sharti zipitie utaratibu wa kuthibitisha kwamba kanuni za kilimohai zimezingatiwa na alama ya ubora kutolewa. Cheti hutolewa kama ithibati kwamba haya yamefanyika.

Kuna mashirika mengi duniani yanoyotoa ithibati kwa bidhaa tofauti tofauti za kilimohai. Afrika Mashariki imebuni kanuni zake za kuthibitisha ubora wa bidhaa zinazokuzwa au kutengenezwa kupitia kilimohai.